
Kiswahili Katika Elimu ya Juu

Wahariri

Ernest Sangai Mohochi
Mwenda Mukuthuria
James Omari Ontieri

Kiswahili Katika Elimu ya Juu

Wahariri

Ernest Sangai Mohochi
Mwenda Mukuthuria
James Omari Ontieri

MOI UNIVERSITY
==PRESS 

Moi University Press, Eldoret Kenya

**©Chama cha Kiswahili cha Afrika Mashariki
(CHAKAMA)**

Haki zote zimehifadhiwa

Kimechapishwa 2019

Sura ya Tisa

Ufundishaji wa Kiswahili Kwa Wakimbizi Katika Kambi za Kakuma na Dadaab: Changamoto na Mwelekeo Mpya

Carren Nyandiba na Isaac Ipara Odeo

Ikisiri

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro (MMUST) kikishirikiana na shirika la Lutheran World Federation (LWF), kinatoa shahada za diploma kwa walimu wakimbizi wanaofundisha katika shule za msingi katika kambi za Kakuma na Dadaab. Kiswahili ni mojawapo ya masomo yaliyoko katika mtaala wa shahada hiyo ambayo wanafunzi hao wanasomea. Sura hii inajadili changamoto za ufundishaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wanaoshiriki katika mafunzo hayo. Aidha, sura hii inatalii mwelekeo mpya uliopatikana kupitia kwa mradi huu, unaoweza kuendeleza ufundishaji wa Kiswahili kwa wakimbizi nchini Kenya.

Utangulizi

Sura hii imetokana na utafiti unaoendelea, kuhusu elimu kwa wakimbizi nchini Kenya. Utafiti huu ulianza baada ya Chuo kikuu cha Masinde Muliro ******(MMUST katika surahii) na shirika la Lutheran World Federation (LWF katika surahii) kutika sahihi mkataba ambao ulilenga kuinua kiwango cha elimu cha walimu wakimbizi katika kambi za Dadaab na Kakuma zilizoko nchini Kenya. Mradi huo ulianza mnamo mwaka wa 2010, na kikundi cha kwanza cha wanafunzi kilifuzu mnano mwaka wa 2012.

Kulingana na ripoti ya UNHCR (2011) utoaji wa elimu kwa wakimbizi ni mojawapo ya shughuli zinazopewa kipao mbele. Ripoti hii inashikilia kwamba elimu ndio ufunguo wa maisha ya baadaye ya wakimbizi, na kwamba mbali na kusaidia katika kuleta amani nchini mwao, elimu huwapa wakimbizi utulivu na amani. Mamlaka ya kutoa elimu kwa wakimbizi yameelezwa katika kipengee cha 22 cha mkataba wa 1951 wa UNHCR, kwamba kila taifa lililotia sahihi mkataba huu litatoa elimu kwa wakimbizi iliyo sawa na ile inayotolewa kwa wananchi wake.

Kwa mujibu wa Kafu (2005), ili kuwepo na maendeleo katika elimu, ni sharti mwalimu akuzwe na kuendelezwa. Richards na Nunan (1990) wanashadidia hoja ya walimu kuendelezwa kwa kufasili maendeleo ya mwalimu kama mfumo unaoendelea wa kumkuza mwalimu kiakili, kitajriba na kimwelekeo. Wanasema kwamba maendeleo ya mwalimu yanaweza kufanywa kupitia kwa mafunzo kabla ya kuanza kuhudumu na mafunzo ya kuongezea ujuzi wanapohudumu. Shirika la LWF linazingatia hoja hii kwamba walimu wanapaswa kupewa mafunzo ya kuimarisha ujuzi wao, ndipo likadhamini mafunzo hayo ya kutoa shahada ya diploma kwa ushirikiano MMUST kwa walimu wenye vyeti vya P1.

Shirika la LWF

LWF ni shirika la kimataifa lisilokuwa na kiserikali ambalo makao yake makuu yanapatikana mjini Geneva Uswizi. Katika kanda ya Afrika Mashariki, shirika hili linatoa huduma katika nchi ya Kenya na Djibouti, ambapo makao makuu ya kanda hili ni Nairobi Kenya. LWF pamoja na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali hupewa mamlaka ya kutoa huduma kwa wakimbizi na shirika la UNHCR. Nchini Kenya, LWF hutoa huduma mbalimbali kwa wakimbizi katika kambi za Kakuma na Dadaab. Mojawapo ya huduma ambazo LWF inatoa katika kambi hizi ni elimu. Katika kambi ya Kakuma, LWF inasimamia elimu katika shule za msingi na za upili ilhali katika kambi ya Dadaab, inasimamia elimu katika shule za chekechea na za msingi katika kambi mbili kati ya kambi tano zilizoko Dadaab.

Asilimia 90 ya walimu wanaofundisha katika shule za wakimbizi ni wakimbizi wenyewe ambao wana kiwango cha elimu cha kidato cha nne au zaidi. Walimu hawalipwi mshahara, bali hupewa fedha kidogo za kujikimu. Mpango huu wa kuwashirikisha wakimbizi kama walimu katika shule ni njia mojawapo ya kuwashughulisha wakimbizi na pia njia ya kuwafanya wakimbizi kujipatia mapato kidogo, mbali na kupunguza uhalifu miongoni mwao. Mnamo mwaka wa 2010, LWF kupitia kwa mamlaka ya UNHCR iliona haja ya kuinua viwango vya walimu wanaofundisha katika shule za wakimbizi. Haja hii ilitokana na sababu kadhaa. Kwanza, matokeo ya mitihani katika shule za wakimbizi yalikuwa duni na yasiyoridhisha licha ya juhudu za kuwekeza katika elimu. Sababu ya pili ni kwamba, ingawa walimu walikuwa wamehudhuria makongamano na mafunzo ya muda mfupi ambapo walipewa vyeti, vyeti hivyo havikuwa vya kitaaluma, na kwa hivyo havingetumika nje ya kambi hizo. Sababu ya tatu ni kwamba UNHCR ilitaka walimu wapate elimu ya kitaaluma ambayo ingewaruhusu wapewe vyeti maalum ambavyo vingeweza kutumika hata wakirudi makwao au wakipata makao katika nchi nyingine.

Ni kutokana na haja hii ambapo Chuo Kikuu cha MMUST kilituma pendekezo la kutoa mafunzo ambayo yangewawezesha walimu kupewa diploma katika elimu ya msingi. Mafunzo hayo kuchukua mwaka mmoja, na hujumuisha masomo matano yanayotahiniwa katika shule za msingi. Masomo hayo ni Kiingereza, Kiswahili, Hesabu, Sayansi, na Elimu jamii. Mbali na kozi za kiakademia, kuna kozi moja ya kufanya mazoezi ya ufundishaji na nyingine ya kufanya utafiti mfupi. Somo la dini halifundishwi katika mradi huu kwa sababu Chuo cha Masinde Muliro hakina walimu waliohitimu kuweza kufundisha dini ya Uislamu ambayo, wanafunzi wengi wakimbizi huisomea. Kikundi cha kwanza cha wanafunzi kilianza mafunzo mnamo mwaka wa 2011 na kumaliza mafunzo mnamo mwaka wa 2012. Kikundi cha pili kuhudhuria darasa mnamo mwaka wa 2013, na wanaendelea na masomo yao, wakitarajiwa kukamilisha kufikia mwisho wa mwaka wa 2014.

Elimu katika Kambi ya Kakuma

Katika kambi ya Kakuma, LWF inasimamia elimu ya shule za msingi na za upili katika kambi ndogo zote. Wakimbizi katika kambi hii wanatoka katika mataifa mbalimbali kama vile Somalia, Ethiopia, Uganda, Sudan Kusini, Rwanda, Burundi na wachache kutoka mataifa ya Afrika Magharibi kama vile Liberia na Cameroun. Wakimbizi wangawanywa na kuishi katika kambi ndogo ndogo kulingana taifa ambapo wanatoka kwa sababu ya tamaduni zinazotofautiana. Kwa sababu hiyo, shule vile huwa na mgawanyiko huo wa wanafunzi. Walimu hao hufundisha katika shule za kambi wanakoishi. Kwa sababu ya hali ilivyo katika kambi hizi na uhaba wa walimu wanaofahamu Kiswahili barabara, iligunduliwa kwamba Kiswahili ni mojawapo ya masomo ambayo matokeo yake yalikuwa duni hasa kilipolinganishwa na masomo mengine. Hali hiyo ilifanya LWF kuwaajiri walimu Wakenya ili kufundisha Kiswahili kuanzia mwaka wa 2010. Hata hivyo, idadi ya walimu wa Kiswahili bado ni ndogo mno ikilinganishwa na idadi ya shule na wanafunzi katika shule hizo.

Elimu katika Kambi ya Dadaab

Kambi kuu ya Dadaab inazo jumla ya kambi ndogo tano, na wakimbizi wanatoka katika nchi za Somali, Ethiopia, Sudan Kusini. Na wachache kutoka Jamhuri ya Kongo, Rwanda na Burudi. Asilimia kubwa ya wakimbizi katika kambi kuu ya Dadaab ni Wasomalia. Tofauti na katika kambi ya Kakuma ambapo LWF inasimamia elimu katika shule za msingi na upili katika kambi zote, katika Dadaab, LWF inasimamia elimu katika kambi mbili tu. Aidha haisimamii elimu katika shule za upili bali husimamia elimu katika shule za chekechea na za msingi. Wanafunzi katika kambi hizi vilevile huenda katika shule kulingana na kambi wanapoishi. LWF ilipoajiri walimu wa Kiswahili katika kambi ya Kakuma, ilifanya hivyo pia katika

kambi ya Dadaab, ambapo walimu Wakenya walijiririwa ili kufundisha Kiswahili katika shule hizo za wakimbizi. Idadi ya walimu walioajiriwa bado ni ndogo, na kwa sababu hiyo. Walimu hao hufundisha zaidi madarasa ya saba na nane, nao walimu wakimbizi wakiachiwa kufundisha Kiswahili katika madarasa ya chini.

Mbinu za Utafiti

Mbinu zilizotumika katika kukusanya data ya utafiti huu ni mahojiano na hojaji. Hojaji zilitumika kukusanya data kutoka kwa wanafunzi wote waliokuwepo katika darasa la 2010/2011. Jumla ya wanafunzi 160 walipewa hojaji kujaza, 100 kutoka darasa la Dadaab na 60 kutoka darasa la Kakuma. Aidha, tulifanya mahojiano ya kina yaliyoshirikisha jumla ya wanafunzi 20, 10 kutoka darasa la Kakuma na 10 kutoka kwa darasa la Dadaab. Mahojiano yalilenga kutambua mielekeo ya wanafunzi kuhusu ujifunzaji wa Kiswahili, ilhali hojaji zilitumika katika kufahamisha viwango vya elimu vya washiriki, umri wao, nchi walizotoka na vilevile maoni yao kuhusu ujifunzaji wa Kiswahili.

Changamoto za Ufundishaji wa Kiswahili

Kukingana na Ur (1992), ufundishaji wa lugha ni mfumo changamano ambao unaweza kugawanywa katika sehemu zifuatazo: kwanza ni utoaji na uelezaji wa dhana ngeni, pili ni utoaji wa nafasi ya utekelezaji na tatu ni kutahini. Ni jukumu la mwalimu wa lugha kuhakikisha sehemu hizi tatu zinashughulikiwa kikamilifu. Wanjala na Kavoi (2013) nao wanafafanua stadi nne muhimu zinazozingatwa katika ufundishaji wa lugha. Stadi hizo ni kusikiliza kuongea, kusima na kuandika. Kila mojawapo ya stadi hizi ni muhimu na huchangia asilia fulani katika ujifunzaji wa lugha. Utafiti huu uligundua kwamba kuna ugumu wa kuzingatia stadi hizo muhimu katika ufundishaji wa Kiswahili miongoni mwa changamoto zingine. Baadhi ya changamoto zinazokumba ufundishaji wa Kiswahili ni kama zifuatazo:

Wanafunzi kutoka Nchi Tofauti

Wanafunzi walioko katika mradi huu wanatoka katika nchi tofauti na wengine wao walihudhuria elimu ya shule za msingi na upili katika nchi zao. Kwa sababu hiyo, kuna wale ambao hawakuwahi kusoma Kiswahili katika shule za msingi na upili. Kwa mfano, wakimbizi kutoka Ethiopia, Somalia, Rwanda na Sudan Kusini. Ufundishaji wa wanafunzi hawa huwa mgumu kwa sababu msingi wao wa Kiswahili ni hafifu. Kiswahili wanachokifahamu ni kile ambacho wamejifunza katika mawasiliano yao kambini na hiki huwa si Kiswahili sanifu. Mwalimu anapofundisha wanafunzi hao, huwa na ugumu sana.

Kufundisha Kiswahili kwa Kiingereza (?)

Wengi wa wanafunzi walioshiriki katika elimu hii hawana umilisi wa Kiswahili hivi kwamba hawaelewi barabara Kiswahili. Wanafunzi walimtaka mwalimu afundishe Kiswahili, huku akitoa maelezo kwa Kiingereza. Hali hii ilitokana na sababu kwamba wengi wao hawakuwa wamepata mafunzo ya kutosha katika shule za msingi na za upili. Hali ilivyo katika shule za wakimbizi ni kwamba Kiswahili hakifundishwi katika madarasa ya chini, huanza kufundishwa katika darasa la 6 hadi 8. Hali hii inawafanya wanafunzi hao kutopata mafunzo ya kutosha, hivyo kuanguka mitihani. Katika shule za upili, ingawa wanafundishwa Kiswahili, wengi wao tayari huwa wamekichukia Kiswahili na kuchukulia somo la Kiswahili kama gumu. Kwa hivyo, huwa pia hawafanyi vyema katika mtihani wa kidato cha nne. Wanafunzi waliopitia mfumo huo wa elimu ndiyo walikuwa katika darasa la diploma, na ilikuwa changamoto kwa mwalimu wa somo la Kiswahili.

Mielekeo ya Wanafunzi

Wengi wa wanafunzi walioshiriki katika elimu hii walikuwa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili. Mielekeo hiyo ilichangiwa na matarajio yao kama wakimbizi. Wengi hutarajia kwamba wanaweza kupata fursa ya kupata uraia katika nchi za ng'ambo kama vile Marekani, Canada, Australia na hata bara Uropa. Kwa sababu ya matarajio hayo, wanafunzi hukupuuza Kiswahili na badala yake kufanya kila juhudi za kujifunza Kiingereza kwani hudhani kwamba kitawafaa zaidi watakapohamia katika nchi za ng'ambo..

Kutozingatia Stadi Muhimu

Wanjala na Kavoi (2013) wanadai kwamba fundishaji wa lugha kupaswa kuzingatia stadi nne kuu, yaani kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika. Ilibainika wazi kwamba walimu wanaofundisha Kiswahili kwa wakimbizi katika shule za msingi na upili hawakuzingatia stadi hizi muhimu. Wanafunzi wengi hawakuweza kuongea wala kuandika sentensi sahihi za Kiswahili, Kwa vile msingi wao katika Kiswahili ulikuwa hafifu, ilikuwa vigumu kwa mwalimu katika kiwango elimu ya diploma kufundisha masuala ya kimsingi ambayo yangeshughulikiwa katika viwango vya shule za msingi na upili.

Uhaba wa Walimu wa Kiswahili

Utafiti huu uligundua kwamba asilimia kubwa ya walimu waliofundisha katika shule za wakimbizi hawakuwa wamepata mafunzo yoyote rasmi katika taaluma ya Kiswahili. Wengi wa walimu ni wanafunzi waliosoma hadi kidato cha nne, ndio hupewa kazi

ya kufundisha katika shule hizo za wakimbizi. Idadi ya walimu waliopata mafunzo rasmi katika Kiswahili ni wachache mno. Hali iliyoko katika shule za wakimbizi ni kwamba viwango vya ubora katika elimu havizingatiwi ipasavyo, hali inayochangia katika walimu wasio na ufasaha katika Kiswahili kuruhusiwa kufundisha Kiswahili katika shule za msingi za wakimbizi.

Uhaba wa Vitabu

Utafiti huu uligundua kwamba shirika la LWF na wafadhili wengine hununua vitabu vya kiada kwa wanafunzi ambavyo vinahifadhiwa shuleni. Ilibainika pia kwamba wazazi hawawanunulii wanao vitabu vya kutumia nyumbani kwa sababu ya ukosefu wa fedha ama kwa sababu nyinginezo. Vilevile, ilibainika wazi kwamba wafadhili wengi wanaotoa misaada ya vitabu hutoa vitabu vya Kiingereza. Kwa sababu hizo, wanafunzi hawana vitabu vya ziada na hata vya hadithi ambavyo wanaweza kusoma wakiwa nyumbani ili kuendeleza ujifunzaji wao wa Kiswahili.

Elimu ya Madrasa

Katika kambi ya wakimbizi ya Dadaab, baadhi ya wazazi hawaruhusu watoto wao kuhudhuria shule za kawaida. Wazazi hawa huwapeleka wanao katika madrasa ambapo wanapata elimu ya dini pamoja na masomo mengine kama vile hesabu na Kiarabu. Katika madrasa, Kiswahili hakifundishwi. Baadhi ya wanafunzi wanaopokea mafunzo hayo ya madrasa ni walimu katika shule za kawaida, na kwa sababu hiyo walikuwa miongoni mwa wanafunzi waliojiunga na mafunzo yaliyotolewa na MMUST. Kiwango cha umilisi wa Kiswahili cha wanafunzi hawa huwa cha chini mno, na wanachangia katika kufaya ufundishaji wa Kiswahili kuwa mgumu.

Mwelekeo Mpya katika Ufundishaji wa Kiswahili

Mbali na changamoto nyingi zinazokumba ufundishaji wa Kiswahili kwa wakimbizi, kuna mwelekeo mpya uliopatikana unaoweza kuchangia katika maenezi na maendeleo ya Kiswahili.

Kiswahili Kufundishwa Somalia na Sudan Kusini

Baadhi ya wanafunzi walioshiriki katika utafiti huu walikuwa na matumaini ya kufuzu na kurudi nchini kwao baada ya amani kupatikana. Wanafunzi kutoka Somalia walisema kwamba mfumo wa elimu wa Kenya umepenya hadi nchi yao na kwamba baadhi ya shule hasa za kibinafsi hufuata mtaala wa Kenya. Hii ni nafasi nzuri sana ambayo lugha ya Kiswahili imepata ya kuweza kuenezwa, kuendelezwa na kusambazwa.

Wanafunzi kutoka Sudan Kusini nao walisema kwamba wana matumaini kwamba wakirudi kwao, wataendelea kuongea Kiswahili, na hata kuwafundisha watu kutoka nchi yao ambao huja Kenya kwa minajili ya shughuli mbalimbali.

Kiswahili Kufundishwa katika Madarasa ya Chini

Kwa muda mrefu, Kiswahili katika shule za wakimbizi kilianza kufundishwa katika darasa la sita hadi nane. Hata hivyo, tangu walimu Wakenya kuajiriwa ili kufundisha Kiswahili katika madarasa hayo ya juu, walimu wakimbizi wamepata fursa ya kufundisha Kiswahili katika madrasa ya chini. Kuna matumaini kwamba baada ya miaka michache, kitaanza kufundishwa katika shule za chekechea kama ilivyo katika sehemu zingine nchini Kenya.

Kiswahili Lugha ya Uhuru

Krashen (1988) anadai kwamba mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha wanayojifunza huchangia katika ujifunzaji wao wa lugha hiyo. Anaendelea kusema kwamba mielekeo kuhusu manufaa ya lugha wanayojifundisha huwasukuma wanafunzi kufanya vyema katika mafunzo ya lugha hiyo mbali na kuizunguza barabara. Baadhi ya wanafunzi walioshiriki katika utafiti huu walisema kwamba ingawa kwa muda mrefu wakimbizi walipuuza Kiswahili kwa vile hawakuona umuhimu wa kukifahamu, hali hiyo imeanza kubadilika. Wakimbimbizi wengi, hasa wale wa kutoka nchi ya Somalia wameanza kujifundisha Kiswahili kwa matarajio ya kuweza kupata makao nchini Kenya na hata kupata vitambulisho vya Kenya. Hii ni kwa sababu waligundua kwamba mara nyingi wasomali wa Kenya na wale wa Somalia hutofautishwa kupitia kwa Kiswahili, yaani wale kutoka Kenya wanaongea Kiswahili, ilhali wale kutoka Somalia hawawezi kuongea Kiswahili. Kwa hivyo, wanakichukulia Kiswahili kama lugha ya kujipatia uhuru kutoka kwa kambi za wakimbizi.

Hitimisho

Sura hii imeangazia changamoto za ufundishaji wa Kiswahili kwa wakimbizi katika kambi za Kakuma na Dadaab. Kutokana na mjadala uliondelezwa, imebainika wazi kwamba Kiswahili kama somo linalofundishwa katika mtaala wa elimu chini Kenya ni somo muhimu na kwa hivyo ufundishaji wake unapaswa kutiliwa maanani. Aidha, mjadala huu umebainisha kwamba Kiswahili kama lugha ya mawasiliano ina nafasi ya kuwa lugha ya mawasiliano mapana hasa katika kanda la Afrika Mashariki, kama anavyopendekeza Inyani (2006). Pia, lugha ya Kiswahili ina nafasi muhimu ya kutumika kama chombo cha kuwaunganisha na kuwatambulisha Waafrika. Japo changamoto za ufundishaji wa Kiswahili ni nyingi, imedhihirika kwamba

kuna mwelekeo mpya kuhusu ufundishaji wa Kiswahili. Tunapendekeza kwamba wataalam, wapenzi wa Kiswahili na wakereketwa wote watafute mbinu za kuweza kushirikiana na mashirika yanayotoa elimu ya wakimbizi ili waweze kutalii namna ufundishaji wa Kiswahili unaweza kuendelezwa na kuboreshwa.

Marejeleo

- Inyani, K. S. (2006). Kiswahili in East African Education: Challenges and Opportunities. In Kambu-Sure, Mwangi, S. & Ogechi, N.O (eds.) *Language Planning for Development in Africa*. Moi University Press Eldoret.
- Kafu, P. (2005). Challenges of teacher education In the Twenty First Century: The Kenyan Experience. In *The Educator: Vol 1* (9-14).
- Krashen, S. D. (1988). *Second Language Acquisition and Second Language Learning*. Prentice Hall, New York.
- Richards, J. C. & Nunan, D. (1990). *Second Language Teacher Education*. CUP. Cambridge.
- Ur, P. (1992). *A Course in Language Teaching: Theory and Practice*. CUP. Cambridge.
- United Nations Higher Commissioner for Refugees (2011). *Refugee Education: A Global Review* Toronto, UNHCR
- Wanjala, F. S. & Kavoi, J. M. (2013). *Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili kwa Wanafunzi na Walimu*. Serengeti Bookshop Publishers. Mwanza.